

BENKI KUU YA TANZANIA
16 Barabara ya Jakaya Kikwete
S. L. P. 2303
40184 DODOMA
TANZANIA
Simu: +255 22 223 3167
Barua Pepe: botcommunications@bot.go.tz



BANK OF TANZANIA
16 Jakaya Kikwete Road
P.O. Box 2303
40184 DODOMA
TANZANIA
Phone: +255 22 223 3167
Email: botcommunications@bot.go.tz

29 Desemba 2023

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VIFAA CHAKAVU

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa Benki Kuu ya Tanzania itauza kwa njia ya mnada wa hadhara vifaa chakavu yakiwemo magari, pikipiki, mitambo, samani za ofisi, vifaa vya TEHAMA na vifaa vingine katika mikoa ya **Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya, Mtwara** na katika ofisi za Benki Kuu zilizopo **Unguja**.

Maelezo zaidi ya vifaa hivyo ni kama yanavyoonekana hapa chini.

Na.	Kituo	Anuani	Kifaa	Tarehe ya Mnada
1.	Dodoma	Barabara ya 16 ya Jakaya Kikwete 40184, S.L.P 2303, Dodoma.	<ul style="list-style-type: none">• Samani za ofisi• Vifaa vya TEHAMA• Vifaa Vingine	20 Januari, 2024
2.	Dar Es Salaam	Mtaa wa 2 Mirambo 11884, S.L.P 2939, Dar es Salaam.	<ul style="list-style-type: none">• Magari (Toyota Landcruiser, Toyota Coaster, Toyota Rav 4, Nissan Patrol, Mercedes Benz, Toyota Landcruiser Prado na Isuzu FSR)• Mitambo (Forklift)• Samani za ofisi• Vifaa vya TEHAMA• Pikipiki (Honda XL)• Vifaa Vingine	3 Februari - 4 Februari 2024
3.	Zanzibar (Unguja)	Eneo la Gulioni, S.L.P 568, Zanzibar.	<ul style="list-style-type: none">• Pikipiki (Suzuki na Honda XL)• Samani za ofisi• Vifaa vya TEHAMA• Vifaa vingine	10 Februari, 2024
4.	Mbeya	Barabara ya Mahakama, S.L.P 1203, Mbeya.	<ul style="list-style-type: none">• Pikipiki (Honda XL)• Samani za ofisi• Vifaa vya TEHAMA• Vifaa vingine	27 Januari, 2024
5.	Mwanza (Tawi)	Barabara ya Makongoro, S.L.P 1362, Mwanza.	<ul style="list-style-type: none">• Samani za ofisi• Vifaa vya TEHAMA• Vifaa vingine	20 Januari, 2024

6.	Mwanza (Chuo cha Benki)	Mtaa wa Capri-Point, S.L.P 131, Mwanza.	<ul style="list-style-type: none"> • Samani za ofisi • Vifaa vya TEHAMA • Vifaa vingine 	27 Januari, 2024
7.	Mtwara	Barabara ya Makonde, S.L.P 1446, Mtwara.	<ul style="list-style-type: none"> • Samani za ofisi • Vifaa vya TEHAMA • Vifaa vingine 	27 Januari, 2024
8.	Arusha	Barabara ya Makongoro, S.L.P 3043, Arusha.	<ul style="list-style-type: none"> • Samani za ofisi • Vifaa vya TEHAMA • Vifaa vingine 	20 Januari, 2024

MASHARTI YA MNADA

1. Mali itauzwa kama ilivyo na mahali ilipo.
2. Malipo ya vifaa chakavu ni asilimia mia moja (100%) na mteja atatakiwa kuondosha vifaa chakavu alivyonunua siku ya mnada.
3. Mnunuzi wa gari, pikipiki na mitambo atalazimika kulipa papo hapo amana "deposit" isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya bei na atatakiwa kukamilisha malipo yote ndani ya muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuzi na amana iliyolipwa haitarudishwa.
4. Mnunuzi wa gari, pikipiki na mtambo atatakiwa kuondoa/kuchukua mali aliyonunua katika muda wa siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
5. Ruhusa ya kuangalia vifaa itatolewa siku mbili (2) kabla ya mnada husika kuanzia saa nne (4:00) asubuhi hadi saa kumi jioni (10:00).
6. Mnada utanza saa nne (4:00) asubuhi hadi saa kumi jioni (10:00) katika kituo kama ilivyoorodheshwa hapo juu.

**GAVANA
BENKI KUU YA TANZANIA**